



**Bora,  
zinavutia,  
bei nafuu...**

na rahisi kumiliki  
zaidi ya  
anavyofikiria!



**pamoja tunaweza**

# SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

## MRADI WA NYUMBA ZA GHARAMA NAFUU ZINAZOJENGWA NA NHC ENEO LA KIBADA, KIGAMBONI

Shirika la Nyumba la Taifa katika mpango mkakati wake wa miaka mitano 2010/11-2014/15 limejikita katika kuwezesha ujenzi wa nyumba 15,000, ambapo nyumba 10,000 zitakuwa za watu wa kipato cha kati na juu na nyumba 5,000 zitakuwa za watu wa kipato cha chini, idadi ambayo haijawahi kufikiwa na Shirika hili tangu lianzishwe mwaka 1962.

Katika kutekeleza mpango mkakati huo, Shirika limeanza kutekeleza mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya nchini, zitakazouzwa kwa wananchi na mashirika mbalimbali ili kusaidia juhudi za Serikali za kuwapatia nyumba bora watanzania. NHC imeshakopa shilingi za kitanzania bilioni 24 mahususi kwa ajili ya kujenga nyumba hizo.

Hivi sasa katika Jiji la Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zipatazo 292 unaendelea katika mradi wa Kigamboni Housing Estate uliopo Kibada - Kigamboni katika Manispaa ya Temeke, ambao umezinduliwa rasmi tarehe 13 Desemba, 2012 na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Uzinduzi wa Mradi huu wa Kigamboni Housing Estate, unaashiria pia kuanza kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu inayotekelezwa na Shirika katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri za Wilaya hivi sasa.

Uzinduzi wa mradi huu ni utekelezaji wa dhamira ya Shirika la Nyumba la Taifa ya kuhakikisha kuwa watanzania wanapata nyumba bora na za kisasa zenye bei nafuu. Wanunuzi wa nyumba hizi wataishi kwenye maeneo yao kwa kuzingatia mfumo wa sheria ya hati pacha (Unit titles Act 2008). Mfumo huu utawawezesha wakazi kuishi kwa utaratibu wakiongozwa na sheria hiyo ambayo imeundwa kulinda maslahi ya kila mnunuzi.

Katika mradi huu, kuna nyumba za aina mbili ambazo ni nyumba ya vyumba vitatu na ya vyumba viwili. Nyumba ya vyumba vitatu ina ukubwa wa mita za mraba 70 huku nyumba ya vyumba viwili ikiwa na ukubwa wa mita za mraba 56.

**Sifa zingine za nyumba hizi za mradi wa Kigamboni Housing Estate ni pamoja na kuwa na:**

- Chumba kimoja kinachojitegemea kwenye nyumba ya vyumba vitatu
- Kila nyumba ina sebule na sehemu ya kulia chakula
- Ukuta unaotenganisha mipaka kati ya maeneo ya wakazi. \*
- Jiko la nje
- Eneo la zahanati
- Eneo la kucheza watoto
- Eneo la shule ya chekechea
- Eneo la maduka

Aidha, maeneo mengine nchini ambayo maandalizi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu yameanza ni Mvomero (Morogoro), Ilembo (Katavi), Geita, Mkinga (Tanga), Babati (Manyara), Monduli na Longido (Arusha), Unyankuni (Singida), Mtanda (Lindi), Kongwa (Dodoma), Iwambi (Mbeya), Mlole (Kigoma) na Mkuzo (Songea).

Karibu Mikoa yote itakuwepo katika utekelezaji wa Mpango wa kujenga nyumba za gharama nafuu na miradi iliyotajwa hapo juu ni miradi ya awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mkakati huo.

Ili kuweza kufikia lengo la kuwa na nyumba za gharama nafuu, Shirika litakuwa linatumia teknolojia ya ujenzi wa nyumba iliyopo katika eneo husika.

Shirika limejipanga kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mpango huu unafanikiwa kwa asilimia mia moja.

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**  
**“Pamoja Tunaweza”**

\*Kila mkazi anaweza kujenga ukuta wake mwenyewe kulingana na michoro ya eneo lake.




# LEGEND



SEMI DETACHED HOUSES OF 3 BEDROOM (72 UNITS)



SEMI DETACHED HOUSES OF 2 BEDROOM (114 UNITS)



EXISTING MODEL HOUSES



BUNGALOW (6 UNITS)



BOUNDARY



RECREATIONAL SPACE



CONSERVATION AREA TO BE MANAGED BY NHC



PROPOSED TOWN HOUSES KIBADA PHASE II

292

PROPOSED NUMBER OF UNITS TO BE BUILT



Proposed Nursery School



Proposed Dispensary



Proposed Town Houses



Proposed Convenient Store



Proposed Conservation Area to be Managed by NHC



Proposed Play Ground




NSSF HOUSING ESTATE-MTONI KIBADA

PROPOSED HOUSING ESTATE TOWN HOUSES KIBADA PHASE II

Conservation Area to be Managed by NHC





LAND USE DISTRIBUTION	
LAND USE	No.
Residential houses(Units)	292
Convenient Stores	04
Nursery School	01
Dispensary	01
Public Open Space	01
Mul purposeground	01
Bungalow	06

## LEGEND


- 1
CLUSTER-1 COMPRISES OF 31 HOUSES;(62 UNITS)  
10 - 3 BR  
2 - 2BR  
06 - BUNGALOW
- 2
CLUSTER -2 COMPRISES OF 17HOUSES;(34 UNITS) AND 3 MORE TO BE DESIGNED LATER
- 3
CLUSTER-3 COMPRISES OF 18 HOUSES;(36 UNITS) AND TWO(2) VACANT PLOTS TO BE DESIGNED AND BUILT LATER = 36
- 4
CLUSTER-4 COMPRISES OF 14 HOUSES;(28 UNITS) AND ONE(1) VACANT PLOTS TO BE DESIGNED AND BUILT LATER = 29
- 5
CLUSTER-5 COMPRISES OF 13 HOUSES;(26 UNITS) AND TWO(2) VACANT PLOTS TO BE DESIGNED AND BUILT LATER = 28
- PH 2
TOWN HOUSES
- PLAY GROUND, POS  
NURSERY SCHOOL & DISPENSARY  
TO BE DESIGNED AND BUILT LATER
- 292
PROPOSED NUMBER OF UNITS TO BE BUILT



### CLUSTER PLAN FOR PROPOSED KIBADA AFFORDABLE HOUSING PROJECT

ON PLOT No. 237 BLOCK - 11 KIBADA 15118 - CHANGANYIKENI

TEMEKE MUNICIPALITY



**SITE PLAN**



pamoja tunaweza



**FLOOR PLAN**  
FOR: 3 BEDROOM APARTMENT



3D Perspectives ,For 3 Bedroom





3D Perspectives ,For 2 Bedroom



# Bora, zinavutia, bei nafuu

**... na rahisi kumiliki zaidi ya unavyofikiria!**

NHC inajivunia kuwaletea nyumba za bei nafuu zilizoko ndani ya eneo tulivu la Kibada-Kigamboni. Kigamboni Housing Estate ipo katika eneo linalofikika kirahisi, kilomita 17 kutoka Feri. Kigamboni Housing Estate ni mradi wa nyumba 182 zilizopangwa kwa kuzingatia vigezo vya miji ya kisasa yenye huduma za msingi zikiwemo sehemu za kuchezea watoto na shughuli mbalimbali za jumuiya, barabara pana inayotoa fursa kwa watembea kwa miguu na baiskeli kuwa huru, vilevile imezingatia nafasi ya miundombinu kama vile mitaro na umeme.



pamoja tunaweza



# Hatua 10 rahisi za kumiliki nyumba yako leo.

1. Chukua fomu ya kununua Nyumba kutoka ofisi yoyote ya mkoa popote nchini au kwenye tovuti ya shirika.
2. Rudisha fomu iliyojazwa ikiwa na uthibitisho wa kulipiwa na malipo ya 10% (ikiwa na VAT) ya thamani ya Nyumba husika.
3. Maombi yako yatatipiwa kwa umakini ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika uchaguaji wa watu wanaostahili kulingana na Vigezo na masharti ya NHC.
4. Kama umefanikiwa, utatumiwa barua ya kuthibitishiwa kukubaliwa maombi yako. Barua zitatolewa kwa wote waliokidhi Vigezo vilivyowekwa.
5. Utatakiwa kulipa 90% iliyobaki kulingana na thamani ya nyumba husika ndani ya siku 90 tangu umepewa.
6. Endapo ukishindwa kulipa ndani ya siku 90, NHC itatoa nyumba kwa Waombaji waliopo kwenye orodha ya wanaosubiri.
7. Orodha ya wanaosubiri itakuwa na majina ya waombaji waliolipa malipo ya mwanzo lakini wakakosa nafasi kwa kuwa nyumba zote zilishapata watu.
8. Kama ukishindwa kulipia kiasi kilichobakia, au ukakosa nafasi ukiwa kwenye orodha ya wanaosubiri, kiasi cha 10% kilicholipwa kinaweza kutumiwa kulipia kwenye miradi mingine ya NHC na waliopo kwenye orodha ya wanaosubiri au kurudishiwa pesa zao.
9. Mauzo ya nyumba za mradi husika yatatangazwa yamefungwa pindi Waombaji waliofanikiwa kupata nyumba wamemaliza kufanya malipo yao yote.
10. NHC itafanya utaratibu wa kutafuta hati za nyumba na kisha kuwapatia wanunuzi walioweza kulipia pesa zote taslimu au kupitia taratibu za mkopo.

## Utaratibu wa malipo:

Mnunuzi wa nyumba anaweza kununua nyumba kwa kupitia taasisi za fedha ambazo shirika linashirikiana nazo au anaweza kulipia nyumba yake kwa utaratibu maalum wa mpaka mwaka mmoja.



pamoja tunaweza



**pamoja tunaweza**

Nyumba chache zinauzwa. Kumiliki nyumba yako leo  
piga: 0754 444 333 au tutumie baruapepe [sales@nhctz.com](mailto:sales@nhctz.com)  
Tovuti: [www.nhctz.com](http://www.nhctz.com), [www.facebook.com/nhctz](https://www.facebook.com/nhctz)

Nyumba hizi zinauzwa chini ya Sheria ya Hati Pacha ya Mwaka 2008 | Vigezo na Masharti kuzingatiwa